

ASb
approved




Kuku Na Jongoo

Brigid Simiyu

Magriet Brink

Kiswahili





Kuku na Jongoo walikuwa marafiki.



Walienda kucheza mpira wa miguu.




Kuku alikuwa golikipa.



Jongoo alifunga bao.




Kuku alikasirika sana.



Kuku aliamua kummeza Jongoo.



Kuku alipoondoka uwanjani, alikutana na Mama yake Jongoo.



Jongoo aliyemezwa alilia, "Mama nisaidie. Nimemezwa."



Jongoo alikuwa na ladha mbaya sana. Kuku alihisi kutapika.



Kuku alikohoa kumtema Jongoo.



Jongoo alipotemwa, alitoroka na kwenda zake.



Kuku na Jongoo walikuwa maadui tangu siku hiyo.

You are free to download, copy, translate or adapt this story
and use the illustrations as long as you attribute in the
following way: Winny Asara Author - Winny Asara

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Magriet Brink

Language - Kiswahili

Level - First words © African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

